HOTUBA YA MHE. SAIDI M. SADIKI, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA WADAU WA ZAO LA KAHAWA, KANDA YA KILIMANAJARO NA TANGA TAREHE 04 MEI, 2017

- Katibu Tawala wa Mkoa;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Wakurugenzi wa Halmashauri;
- Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa;
- Ndugu Mwenyekiti wa Kamati ya Kanda ya kuendeleza Kahawa;
- Ndugu Wataalamu na Watendaji;
- Ndugu wana-Habari;
- Wageni Waalikwa;
- Mabibi na Mabwana:

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutanika tena hapa leo, sote tukiwa na afya njema.

Pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kamati ya wadau wa kahawa kanda ya Kilimanjaro na Tanga pamoja na bodi ya Kahawa kwa kunialika na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo ili tuweze kujadili njia bora ya kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na umaskini hasa kwa kuangalia changamoto zinazokabili sekta ya kahawa ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa mikoa yetu ya kanda ya Kilimanjaro.

Aidha napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisheni nyote katika mkutano huu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo cha kahawa katika Mikoa yetu na nchi kwa ujumla.

Mkutano huu wa leo ni muhimu sana siyo tu kwa Wadau mliojumuika hapa, bali ni kwa wananchi wote wa mkoa wa Kilimanjaro na Tanga. Hii inatokana na ukweli kwamba kabla ya kuanguka kwa kilimo cha kahawa, kilimo hiki kilikuwa ni kati ya shughuli kuu zilizokuwa zinawaingizia wananchi wengi wa Mikoa yetu hasa Kilimanjaro kipato kikubwa, kilichowawezesha wananchi wake kusomesha watoto wao, kuboresha makazi, kujipatia fedha kwa chakula na mahitaji mengine muhimu ya maendeleo.

Aidha umuhimu wa zao la kahawa si kwa mikoa hii pekee bali ni kwa taifa zima kwani linachangia kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni ikiwa ni mojawapo ya mazao makuu ya asili ya biashara ambapo linachangia wastani wa asilimia 5 ya thamani ya mauzo ya bidhaa zinazouzwa nje na asilimia 24 ya thamani ya mauzo yanayotokana na mauzo ya mazao ya asili. Takwimu za dola za kimarekani zilizoingizwa nchini kwa miaka mitatu ni kama ifuatavyo:

Mwaka 2013/14 kahawa iliingizia Taifa jumla ya dola za kimarekani 135,768,630, mwaka 2014/15 dola 136,096,087 na mwaka 2015/16, dola 127,038,824.

Ndugu Wajumbe;
Pamoja na umuhimu wa sekta ya kahawa katika uchumi wa mkoa na taifa, kuna **changamoto nyingi** ambazo zimejitokeza na kutishia maendeleo ya kilimo cha Kahawa katika mikoa yetu. Changamoto kubwa iliyojitokeza ni kuporomoka kwa uzalishaji wa kahawa kulikosababishwa na:

- Kuyumba kwa bei na wakulima kukata tamaa ya kuyatunza mashamba yao;
- Kuyumba kwa ushirika ukiongozwa na chama kikuu (KNCU) ambacho kwa miaka mingi ndiyo kilikuwa tegemeo la wakulima wa kahawa.
- Ukosefu wa pembejeo za uhakika na zenye ubora;
- Magonjwa na wadudu wanaoshambulia kahawa;
- Miti ya kahawa kuwa na umri mkubwa;
- Kupungua kwa rutuba ya udongo kutokana na kilimo cha muda mrefu kisichozingatia kanuni za kilimo bora;
- Mabadiliko ya tabia nchi yaliyosababishwa na uharibifu wa mazingiza;
- Uzalishaji na tija ndogo inayotokana na wakulima wadogo kutokuzingatia kanuni za kilimo bora cha kahawa;

- Mashamba ya Ushirika yaliyokuwa ya Masettler kutotumika ipasavyo kwa mujibu wa mkataba na maagizo ya Serikali;
- Kituo cha Utafiti wa zao la kahawa (TaCRI) kutopewa umuhimu unaotakiwa kwani kimeachwa kama yatima;
- Kubadilishwa kwa matumizi ya ardhi ya kilimo cha kahawa na kuwa ya makazi.
- Baadhi ya mashamba makubwa kutowekeza sana kwenye zao la kahawa na kuhamia kwenye mazao mengine.

Ndugu Wajumbe;
Kuyumba kwa ufanisi katika Kilimo cha kahawa kanda yetu kumeleta madhara makubwa katika vita yetu ya kuondoa umasikini na pia kumeathiri sana uchumi wa kanda yetu ya kahawa ya Kilimanjaro. Ni mategemeo yangu kuwa kupitia mkutano huu tutapata fursa nzuri ya kujadili kwa kina changamoto hizi na baadhi ya matatizo ya msingi ambayo yamekuwa yanakwamisha maendeleo ya zao la Kahawa katika kanda hii na kuyapatia ufumbuzi yale ambayo yako ndani ya uwezo wetu kama wadau, na kutoa mapendekezo kwa serikali kwa yale ambayo yanahitaji serikali kuyafanyia kazi.

Ndugu Wajumbe;
Mikutano na warsha nyingi kuhusu kilimo zimekuwa zikifanyika bila kuleta mafanikio ya kutosha. Ningependa kuona mkutano huu unakuwa wa tofauti na wenye tija. Ni matarajio yangu kuwa,

baada ya kusikiliza mada zitakazotolewa na kuzijadili kwa kina, tuweke mikakati madhubuti na inayotekelezeka itakayotuwezesha kufufua na kuendeleza sekta ya kahawa katika mikoa yetu na taifa kwa ujumla. Napenda sote tuone umuhimu huu hasa tukiunganisha nguvu zetu kwa pamoja na kuhakikisha kuwa tunatumia vizuri taasisi ya utafiti ya zao la kahawa (TaCRI) iliyopo katika mkoa wetu wa Kilimanjaro.

Ndugu Wajumbe;

Kwanza; kabisa kuna umuhimu kwa wadau wote tulioko hapa kufanya tathmini ya kina kuhusu matatizo yanayolikabili zao la kahawa katika mikoa yetu na kanda ya kaskazini kwa ujumla wake na kupendekeza hatua za msingi za kuchukuliwa. Kahawa inayozalishwa kilimanjaro ndiyo nembo ya uzalishaji wa Kahawa katika nchi yetu hivyo si vema nembo hii kuachwa kupotea kwani si tu itaathiri wakulima wa Mikoa yetu bali wakulima wa kahawa Tanzania nzima kwa ujumla wake.

Pili; kuongezeka kwa uzalishaji wa kahawa ni lazima kuende sambamba na kupatikana kwa soko la uhakika. Soko la kahawa ni pamoja na kuhamasisha soko la ndani kwa matumizi ya kahawa pamoja na bidhaa zake. Kwa mfano, iwapo nusu ya idadi ya wana Kilimanjaro wote watakunywa angalau **kilo moja** tu ya kahawa kwa mwaka, kiwango kikubwa cha kahawa inayozalishwa katika mikoa yetu hii itakuwa

tumeitumia wenyewe na sisi wananchi kupata faida zitokanazo na unywaji wa kahawa. Hivyo, kahawa inabidi itumike kwa wingi zaidi katika mahoteli, tafrija na sehemu mbalimbali za vinywaji nchini ili kuongeza matumizi ya kahawa kwa ujumla.

Tatu; kwa zao lolote kuwa na mafanikio ni lazima kuwepo na utafiti wa kina ambao utasaidia kupata mbegu bora/miche bora na mbinu mbalimbali za kupambana na magonjwa na wadudu. Kwa hiyo ni muhimu kwa Mkutano wetu kujadili changamoto na kutafuta njia endelevu za kuhakikisha upatikanaji wa miche bora hasa inayostahimili magonjwa na ukame pamoja na kuhakikisha huduma bora za ugani zinazohusu zao la kahawa zinawafikia wakulima kwa muda muafaka na kupandwa

Nne; kuweka jitihada za kuhamasisha kupanda kwa bei ya kahawa na kuhakikisha uzalishaji unaongezeka, jambo ambalo ni lazima liendane na juhudi za kuhakikisha ubora wa kahawa unaongezeka kwa ujumla na kuendeleza jina zuri la kahawa ya Tanzania katika masoko ya kimataifa kwani ndiyo njia pekee na endelevu ya kuhakikisha sekta hii inarejea katika hali yake ya zamani au zaidi.

Tano; nimeambiwa kuwa kufuatia mabadiliko ya sheria ya mwaka **2009** inayounda bodi za mazao, mikutano hii ya wadau imerasimishwa na kuifanya kuwa ya kisheria kwa kuwa inawapa fursa wadau

kukutana na kuzungumza juu ya mustakabali wa sekta ya kahawa. Hivyo na waasa wadau wa kahawa kutumia fursa hii vizuri kwani siku zote majadiliano ndiyo yanayoleta maelewano na kuondoa mivutano isiyo ya lazima ndani ya sekta ambayo wote mna maslahi**.** Ustawi wa sekta ya kahawa ni faida kwa wadau wote wa kahawa na Taifa kwa ujumla.

Sita; tuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji kwani kahawa inahitaji maji ya kutosha ili iwe na uzalishaji wa kutosha.

Mwisho;
Ingawa yapo mambo mengi ambayo yanatakiwa kuzungumzwa kuhusu zao la kahawa, ningependa haya niliyoyataja tuyazungumze na kuhakikisha tunayatolea majibu na kuyawekea mikakati ili tunapotoka hapa kila mmoja wetu awe ameelewa njia sahihi ya kutekekeza tuliyoyajadili na kila mmoja wetu akatekeleze wajibu wake kwa nafasi yake katika kuendeleza zao la kahawa katika kanda yetu ya Kilimanjaro.

Baada ya kusema haya machache, sasa napenda kutamka kuwa; **mkutano wa wadau wa Zao la Kahawa kwa Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga, mwaka 2017 umefunguliwa rasmi.**

Ahsanteni Sana kwa Kunisikiliza!